## NASAHA ZA WIKI



NA NKWAZI MHANGO
nkwazigatsha@yahoo.com

# Itafutwe suluhu badala ya kutaifisha mifugo

TAARIFA kuwa ng'ombe 3,083 zilitaifishwa na Serikali hivi karibuni baada ya kukutwa kwenye mbuga ya Wanyama ya Tarangire, siyo habari nzuri si kwa wafugaji, wananchi, serikali wala taifa kwa ujumla.

Hivi ni kweli bado tunanyang'anya mifugo kwa kuingia kwenye mbuga au hifadhi karne ya 21. Tunamkomoa nani zaidi ya uchumi wetu hasa ikizingatiwa kuwa hao wanyama wanaopigwa mnada huuzwa kwa bei ya kutupwa na mara nyingi hununuliwa na makundi ya wafanyabiashara wanaoshirikiana na waendesha minada? Je hii ni haki kwa wafugaji wetu walioko karibu na mbuga na hifadhi ambazo zimetokea kuwa tishio kwao na mifugo yao?

Ingawa wahusika walikaririwa wakisema kuwa kupiga watuhumiwa faini hakuzuii wao kuendelea kuingiza mifugo yao kwenye maeneo husika, kwanini wasiongeze viwango vya faini au kutafuta njia mbadala na mujarabu itakayohakikisha suluhu inapatikana badala kufilisiana na kuumizana?

Serikali iwatafutie wafugaji maeneo ya malisho hasa ikizingatiwa kuwa kinachoitwa mbuga au hifadhi ni ardhi ambayo, kabla ya kuundwa Tanzania ilikuwa ikitumiwa na wafugaji bila kikwazo chochote. Kimsingi, ni ardhi yao waliyonyang'anywa. Ajabu, aliyewanyang'anya ardhi ya malisho yao sasa anaanza kuwanyang'anya hata mifugo yao na kuongeza uhasama na umasikini.

Hawa waathirika wana akili na maarifa ya namna ya kutunza hata kuharibu wanyama. Kwanini hatuwaangalii hivi? Mtu aliyekwishapoteza vyanzo vyake vya mapato na maisha ana hasara gani akihujumu hao wanyama wasio na akili ya kuweza kutoa ushahidi dhidi yao? Kuendeleza mbinu hatarishi za kunyang'anyana mifugo kunaweza kujenga mazingira hatarishi ambapo watakaolipia ni wanyama hao mnaotaka kuwalinda. Lindeni wanyama na wafugaji kwa pamoja kwa kuweka utaratibu mzuri wa kugawana raslimali hii.

Mbali na kuwadhulumu, unapotaifisha mifugo ya mtu na kuipiga mnada, unamtia umaskini yeye, familia yake, jamii yake hata eneo atokako. Kwani, unamnyima uwezo wa kujikimu na kuchangia kwenye uchumi wa taifa.

Pia, ifahamike, kwa wafugaji, mifugo si utajiri tu kwao bali ni alama yao ya heshima katika baadhi ya jamii. Hivyo, mfugaji anapofilisiwa mifugo yake anaathirika kiuchumi na kijamii. Kutaifisha mifugo ya mfugaji hakuna tofauti na kumuua yeye na jamii yake. Maana, ndiyo kazi anayojua. Ni sawa na kumtoa samaki majini ukategemea aendelee kuishi.

Serikali inashindwaje kuwatafutia wananchi wake maeneo ya kufugia na kulisha mifugo yao? Inakuwaje wenye ng'ombe wakamatwe na kuwekwa ndani? Je hilo ndilo jibu au kufanya watu waichukie serikali yao kutokana na uamuzi na sheria za kikoloni na za kizamani? kumbukeni ni hao waliowapigia au ambao watawapigia kura. Mbona wanyama wanapoingia kwenye makazi ya watu kudhuriwa na waathirika wala serikali kutiwa ndani? Mbona madereva wanapovunja sheria za barabarani hupigwa faini bila kutaifisha magari yao au kwa vile wenye magari wengi ni matajiri na wakubwa kama wakoloni walivyotunga sheria hizi makusudi kujilinda?

Ushahidi unaonesha kuwa wanyama wamekuwa wakiingia kwenye maeneo ya wananchi. Lenani Seyani mmoja wa wafugaji anasema; "sisi na hifadhi sio maadui, kipindi hiki wanyamapori wameanza kuja kwa wingi maeneo yetu ya makazi huku Terati na kwingineko na tumekuwa hatuwadhuru licha ya kuja na magonjwa." Alikaririwa na gazeti moja la kila siku nchini la Desemba 27, 2022.

Hawa ni Watanzania walioamua kufanya kazi ya ufugaji. Kutaifisha ng'ombe zao, licha ya kuonesha ni unyanyasaji, haiisaidii serikali, wananchi wala Tanzania. Nini maana ya kupigania na kupata uhuru sasa? Nadhani serikali yetu ilirithi sheria au mawazo ya kikoloni. Hapa kinachopaswa kufanywa, ni kuelimishana na kutafuta suluhu pamoja, badala ya serikali kujifanya ina haki kuliko wafugaji wakati serikali na nchi ni mali ya Watanzania popote walipo.

Kama ambavyo serikali iliondoa ujinga wa kuzuia watu wa mipakani kuuza mazao nje ya nchi, iondoe haya makatazo ya kuingiza wanyama kwenye mbuga. Kwa mfano Wamasai, huwa hawali nyamamwitu. Hivyo, wapewe mafunzo na vibali juu ya namna ya kuchangia mbuga na hifadhi bila kuleta madhara kama ilivyokuwa kwa miaka milioni nyingi iliyopita kabla ya kuja serikali na mataifa yaliyotengenezwa na mkoloni mwaka 1884.

Nashauri watenge maeneo ya hifadhi na mbuga walau nusu ambapo wananchi wataruhusiwa kuingiza mifugo yao na kulisha huku wakipewa jukumu la kuhakikisha wanyama hawadhuriwi. Huu ni mfumo unaotumika kuondoa migogoro baina ya binadamu na wanyama uliokwishafanyika sehemu nyingi duniani. Mfano, jamii zinazosifika kwa kuwinda na kuua wanyama zinapowezeshwa kiuchumi na kielimu juu ya faida za wanyama na kuona matunda yake, hugeuka kuwa walinzi wazuri wa wanyama kwa vile wana faida kwao na nchi zao. Na wafugaji kadhalika. Wakielimshwa na kupewa jukumu la kusimamia wanyama, watawalinda kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kuingia ukoloni.

CamScanner

to provide education and methods to tender internationally so that many Tanza-

vices to the UN ... serve," Lieutenant Gen Othman said.

# Fishermen counselled on environmental conservation

By DAILYNEWS Reporter

A DAR ES SALAAM University College of Education (DUCE) Senior lecturer in Geography and Economics Department, Dr Emiliana Mwita has urged the fishermen in Somanga, Kilwa District of Lindi Region to use the skills they have to help the society around them and the government in preserving the environment.

Dr Mwita made the call recently when she was handing over the Global Positioning System (GPS) to Somanga fishermen to assist their coral planting activities that will enable an increase in fish in the sea.

The GPS was handed over after DUCE visited the fishermen's activities in Mwamba Fisi and witnessed the challenges they faced.

"We are handing over this GPS to help them in their wealth production activities. They have shown great patriotism for their country and are doing activities to help deal with climate change by volunteering without waiting for the government to do it for them," said Dr Mwita.

She noted that before handing over GPS they used it with fishermen when surveying the sea to see the activities of planting corals and found that the GPS is very important.

"Today we set where we started and we have been able to go one kilometre from where they go to take the corals and plant them," said Dr Mwita, adding it is a big area so we have seen the challenges, especially when using canoes.

She said that the community has become an example because it has been able to know the problems they face and solve them together. She added although they are researchers (DUCE), they have learned a lot and continue to learn more from the Somanga people.

On his part, a Somanga fisherman, Mr Hamis Basha who also used to teach other fishermen, commended DUCE for providing them with the equipment as well as funds to enable them to fulfill their duties to fight climate change.

He said that they cannot hide the knowledge they have from other people since they want to catch fish and do business. Once they hide knowledge, it may cause the fish from other areas to decline, where they will come to compete with them at Kilwa.

"This education really cannot be greedy. For example, if fish are missing from here (Kilwa) or other places, fishermen cannot rest because it is their business. They will be struggling on the islands and other places so that they can earn income and so they can reach Kilwa where we will strive to catch each other. So, we are ready to provide education to our colleagues who want so that fish can reproduce in abundance," Basha said.

CS CamScanner